# MATARAJIO

- Kuongeza uwezo wa utafiti nchini katika utabiri wa mabadiliko ya hali ya hewa na kuchunguza madhara ya mabadiliko ya hali ya hewa rasilimali maji kwa ajili ya kilimo katika nyanja mbalimbali
- Kuongeza uwezo wa utafiti na ushindani katika taasisi mbalimbali Tanzania kwa kuchambua na kupanga mikakati ya kukabiliana na hali inayofaa katika sekta ya kilimo kuhusiana na mabadiliko katika matumizi ya ardhi na upatikanaji wa maji kutokana na mabadiliko ya hali ya
- Tunatagemea wanafunzi watatu wa Ph.D. na watatu katika shahada ya pili(.Msc's degrees)
- Ongezeko la mtandao wa watafiti kati ya Taifa na kimataifa katika nyanja ya mabadiliko ya hali ya hewa na athari zake na jinsi ya kukabiliana na mabadiliko haya katika kuboresha rasilimali watu,mazingira na mali zao.

- Mbinu za kiutafiti –'hydrological and agronomic model' kutumika na kufanyiwa majaribio kwenye bonde la mto Ruaha Mkuu, uwezekano wa kutabiri mabadiliko kwenye maji, rasilimali na uzalishaji wa mazao kama matokeo ya mabadiliko ya hali ya hewa na uwezekano wa marekebisho.
- Kuongeza uelewa na mabadiliko ya hali ya hewa kwa viongozi wa ngazi mbalimbali kutoka ngazi ya juu hadi ngazi ya shina(chini kabisa). Pia kuongeza uelewa kwa wadau mbalimbali wa hali ya hewa, kilimo na mazingira pamoja na vyombo vya habari taifa na kimataifa

# WASHIRIKI WA MRADI:

Wafuataao ni washirika wa mradi huu:

**Denmark:**

- Geological Survey of Denmark and Greenland (GEUS) (main applicant)
- Department of Geography and Geology (DGG), University of Copenhagen (UC)
- Danish Climate Centre (DCC), Danish Meteorological Institute (DMI)

**Tanzania:**

- Institute of Resources Assessment (IRA), University of Dar es Salaam (UDSM)
- Water Resources Engineering Department (WRED), University of Dar es Salaam (UDSM)
- Tanzania Meteorological Agency (TMA)


**Kiongozi Mkuu wa Mradi**
**Dr. Karen G. Villholth (GEUS)-Denmark**
**kgv@geus.dk**

**Kiongozi Mwakilishi wa Tanzania**
**Prof. Pius Z. Yanda (IRA/UDSM)-Tanzania**
**yanda@ira.udsm.ac.tz**


HEKIMA NI UHURU

G E U S



# Athari za Mabadiliko ya Tabianchi katika Rasilimali Maji na Kilimo - na Mikakati ya Kukabiliana Nayo (CLIVET))

# UTANGULIZI

Mabadiliko ya tabianchi ni moja ya mambo yanayotishia maendeleo duniani na hupelekea kupunguza kasi ya maendeleo na kurudisha nyuma maendeleo ya nchi. Kutokana na utafiti uliofanywa na wataalam wa hali ya hewa na Klimatolojia inaonyesha kwamba maeneo mengi duniani yamekumbwa na mabadiliko ya tabianchi. Mabadiliko ya tabianchi yamesababisha ongezeko la ukame, mafuriko, magonjwa na kupanda kwa kina cha bahari, theluji kuyayuka, mfano mlima Kilimanjaro na misimu ya mvua kubadilika. Nchi maskini wameathirika sana na mabadiliko ya tabianchi kwa sababu hawajajiandaa kukabiliana na hali hiyo.Watu wengi wanaishi vijijini ambao msingi wao mkubwa wa maisha ni kilimo cha msimu ambacho kinategemea mvua za msimu. Kutokana na mabadiliko ya tabianchi Tanzania imeanza kuweka mikakati ya kupambana na tatizo hilo mfano ni Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini (MKUKUTA). Mradi wa CLIVET ni mradi uliodhaminiwa na DANIDA. Mradi huu utasaidia kutoa mchango mkubwa hasa katika kutoa taarifa zinazousiana na mabadiliko ya tabianchi na hali ya hewa na jinsi ya kukabiliana na tatizo hilo.

**Figure 1: Organogram of CLIVET**




# KUHUSU MRADI

Tanzania imechaguliwa kuwa eneo la mradi wa CLIVET kwa vile Tanzania nayo imekumbwa na tatizo la mabadiliko ya hali ya hewa kama nchi nyingine duniani. Danida imepanga majukumu yake katika nchi yetu na huu mradi ni mmoja kati ya majukumu ambayo DANIDA imejiwekea hapa nchini katika sekta ya kilimo na mazingira. Mradi huu utasaidia ufanisi, kujifunza na kujenga uwezo wa utafiti na njia za kukabiliana na athari za mabadiliko tabianchi. Mradi huu uliaofadhiliwa na DANIDA umeanza kufanya kazi kuanzia Septemba 2009 na unategemea kumalizika Desemba 2014. Mradi huu utasaidia kuongeza uelewa na kuongeza utaalamu katika masuala ya utafiti na ushindani kati ya taasisi za Tanzania katika kufafanua na kuendeleza mapambano dhidi ya madhara yanayoleta mabadiliko ya tabianchi.

## Malengo ya Mradi CLIVET

Malengo ya jumla ya mradi huu ni kuchangia uwezo katika masuala ya elimu na utafiti Tanzania ili kupambana na athari zitokanazo na mabadiliko ya tabianchi na kutengeneza mkakakati ambao utasaidia Taifa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi hasa katika upande wa maji na matumizi yake na katika sekta ya kilimo.

### Malengo mahsusi ya mradi huu ni:

- Kusaidia ujenzi wa taasisi binafsi na uwezo wa kufanya utafiti wa mabadiliko ya tabianchi na madhara yake katika nyanja za rasilimali maji na shughuli za kilimo.
- Kusaidia kumuwezesha mtu mmoja mmoja na taasisi kujenga uwezo jinsi ya kukabiliana na matokeo ya mabadilliko haya na kuweka mikakati ya kukabiliana nayo
- Kuchangia katika majadiliano ya sera za kitaifa juu ya mwafaka wa mikakati wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi katika usimamiaji wa maji ndani ya sekta ya kilimo
- Kujenga ushirikiano wa utafiti katika mabadiliko ya tabianchi kati ya washirika/wadau wa nchi za Kaskazini na Kusini na kuunga mkono ushirikiano na utafiti wa kimataifa kushughulikia masuala ya mabadiliko ya tabianchi katika sekta ya kilimo.

# MIKAKATI YA UTEKELEZAJI

**Mradi umegawanyika katika sehemu tatu:**

1. Kutabiri na kutathmini mabadiliko ya hali ya hewa katika bonde la mto Ruaha

2. Kutabiri na kuchambua madhara ya mabadiliko ya tabianchi na mikakati ya kukabiliana nayo katika haidrolojia na rasilimali maji ndani ya sekta ya kilimo katika bonde la mto Rufiji nchini Tanzania.

3. kuchambua mabadiliko ya tabianchi na athari zake na kutoa ushauri jinsi gani ya kupambana na athari hizi hasa katika kilimo ili kuweza kuboresha tamko la Mheshimiwa Raisi J.Kikwete la kilimo kwanza

**Figure 2: Eneo la Mradi**

